



Kilimohai Mark

## FAHAMU KUHUSU ALAMA YA KILIMOHAI

### Alama ya Kilimohai ni nini?

Kilimohai organic ni alama inayotumika kuashiria bidhaa husika imezalishwa kwa kufuata viwango wa kilimohai vya Afrika Mashariki vijilianavyo kama East Africa Organic Products Standards. Alama hii inatumika kwa bidhaa za soko la ndani na Afrika Mashariki na hutolewa na mwamvuli wa kilimohai wa nchi husika ambapo kwa Tanzania Shirika la Kilimohai Tanzania (Tanzania Organic Agriculture Movement-TOAM) ina jukumu hilo.

### Ninawezaje kuthibitishwa kwa alama hiyo?

TOAM inatumia mfumo shirikishi wa udhibiti ubora (Participatory Guarantee System-PGS) kuwathibitisha wakulima na wadau wanaoshirikiana nao kufuata viwango vya kilimohai vya Afrika Mashariki kuweza kutumia alama ya kilimohai. Pia TOAM hutoa huduma hiyo kwa wadau wasio kwenye vikundi kama wakulima, wachakataji, wafugaji n.k.

## Ili kuweza kuthibitishwa na TOAM ni muhimu kuzingatia yafuatayo:

1. Una elimu kuhusu mfumo wa kilimohai unaotekeleza: Hii ni hatua ya msingi ambayo TOAM itatakiwa kujiridhisha kuwa mteja anayehitaji huduma ya kuthibitishwa amewahi kushiriki mafunzo ya kilimohai katika mnyororo wa thamani anaoufanyia kazi na hivyo anafahamu viwango vya kilimohai vinahitaji nini.
2. Kama ni kikundi, wawe wamepatiwa mafunzo ya Mfumo shirikishi wa udhibiti ubora ujulikanao kama (PGS) na wanautekeleza.
3. Kutuma maombi ya ukaguzi kwa kujaza fomu maalumu atakayopewa na TOAM ili kukusanya taarifa za mfumo unaotakiwa kuthibitishwa.
4. Afisa ukaguzi kutoka TOAM atatakiwa kufika eneo hilo na kufanya ukaguzi kwa kuzingatia viwango vya kilimohai vya Afrika Mashariki.
5. Rasimu ya kwanza ya ripoti itatolewa na kujadiliwa kwa Pamoja na mteja kuweza kuangalia na kuthibitisha kuwa alichokandika mkaguzi ndicho alichokishuhudia na wakishakubaliana ripoti kamili itatoka.
6. Kama ripoti itaonesha kuwa mfumo uliokaguliwa umefuata viwango vya kilimohai vya Afrika Mashariki muhusika atakabidhiwa cheti na leseni ya kumuwezesha kutumia alama ya kilimohai organic kwenye bidhaa zake kwa kipindi kilichoainishwa kwenye report. Kama ripoti itaoneshwa kuwa bado mfumo husika haujaweza kufuata kwa usahihi viwango vya kilimohai, TOAM haitaweza kutoa cheti na leseni bali itaendelea kushirikiana na mdau/wadau husika kuwezesha kurekebisha maeneo yanayohitaji marekebishi ili waweze kufanikiwa kutekeleza kilimohai kwa usahihi.
7. Baada ya muda wa matumizi ya leseni kuisha muhusika atakiwa kuwasiliana na TOAM na kuweza kuhuisha leseni yake kwa taratibu atakazoelekezwa.

